BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Pili – Tarehe 15 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Nam. 3 ya 2011 na Kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Nam. 3 ya 2011 na Kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

147. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Zanzibar kama nchi, imeshuhudia majanga kadhaa ikiwemo kuzama kwa meli ya 'Mv. Spice Islander' mnamo Septemba mwaka 2011, ambayo ilisababisha upotevu wa maisha na mali. Licha ya Serikali kuunda Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, jitihada za kukabiliana na majanga hasa ya baharini, zinakabiliwa na changamoto nyingi.

(a) Je, ni hatua na mikakati gani inayochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na majanga ya baharini, na hatua zipi za kuzuia majanga kama ya 'MV Spice Islander' yasitokee tena.

(b) Je, ni kikosi gani hasa kilicho na jukumu la kushughulikia majanga ya baharini katika nchi yetu na ni kwa vipi kinatekeleza majukumu yake.

(c) Je, Serikali ina mpango gani bora wa kuvijengea uwezo wa kimafunzo na kuvipatia vifaa vya kisasa vikosi vya KVZ, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Kikosi cha KMKM na vikosi vyengine ili kukabiliana na majanga.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

26. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Wakati wa sherehe za wafanyakazi (May Day, 2023) Mhe. Rais alitoa ahadi kwa wafanyakazi kuwa watalipwa pesa kwa ajili ya nauli za kwenda na kurejea kazini, jambo ambalo liliwapa matumaini makubwa wafanyakazi wote wa Zanzibar.

(a) Kwa nini agizo hilo limekwama hadi hii leo bado halijatekelezwa.

(b) Kwa kuwa agizo hilo la Mhe. Rais ni sawa na amri, Je, hatuoni kuwa kutokutekelezwa kwake ni kuyadharau mamlaka ya Mheshimiwa Rais.

Ofisi ya Kazi, Uchumu na Uwekezaji:

70. MHESHIMIWA ZAINA ABDALLA SALUM (Nafasi za wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa Mabaraza ya Halmashauri na Manispaa ni miongoni mwa taasisi za Serikali zinazokusanya fedha za uwezeshaji kwa wajasiriamali wa makundi maalum, na kwa kupitia makusanyo hayo, hutenga asilimia 1.0. Na kwa kuwa, Wizara yako imeyataka Mabaraza ya Halmashauri na Manispaa husika kulipa fidia ya mkopo kwa vikundi vitakavyoshindwa kulipa.

Je, ni sababu gani za msingi ambazo zimepelekea kuyataka Mabaraza ya Halmashauri na Manispaa ya Wilaya yalipe mkopo wa kikundi ambacho kitashindwa kulipa mkopo na ukizingatia kwamba vikundi hivi ni vya wananchi.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

96. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hapo zamani, Zanzibar ilijivunia umaarufu mkubwa katika ulimwengu wa soka katika eneo lote la Afrika ya Mashariki na Kati.

Je, Wizara inawashirikisha vipi wanamichezo nguli wa zamani katika kuinua mchezo wa mpira wa miguu nchini.

166. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni lini Serikali italifanyia ukarabati jengo la Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kutokana na umuhimu na mchango mkubwa linaloutoa katika harakati za maendeleo ya lugha adhimu ya Kiswahili duniani.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

68. MHESHIMIWA SABIHA FILIFIL THANI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mafanikio makubwa yaliyopatikana juu ya filamu ya 'Royal Tour', ni pamoja na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watalii nchini.

Je, Wizara yako imejipanga vipi kuwasimamia wawekezaji katika sekta ya utalii, ili watoe huduma bora zitakazowafanya watalii hao waridhike na kuwa mabalozi wetu wazuri wanaporudi nchini mwao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

45. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Madarasa mawili ya Skuli ya Maandalizi (TuTu) ya Machengwe katika jimbo la Pandani yalianza ujenzi wake katika mazingira magumu kwa mashirikiano kati ya wananchi, wafadhili, na Serikali. Hata hivyo, ujenzi wa skuli hiyo bado haujakamilika na skuli haijaweza kutumika.

(a) Je, ni lini Serikali itaviezeka vyoo katika skuli hiyo ili viweze kutumika.

(b) Je, ni lini jengo la skuli hiyo litapigwa plasta na kufanyiwa matengenezo ya mwisho.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuipatia samani na kuijenga ofisi ya walimu wa skuli hiyo ili iweze kufunguliwa na kutumika.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

76. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Upandishaji wa bei ya vyakula na bidhaa mbali mbali kiholela, umekuwa ni tatizo kubwa hapa Zanzibar kunakopelekea kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wenye kipato cha chini.

(a) Je, ni lini litatatuliwa tatizo hilo.

(b) Kwa nini tusiwe na bei elekezi tukawa tunazitangaza juu ya kupanda na kushuka kama ilivyo katika bidhaa ya

mafuta hapa nchini.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusu kuwapunguzia makali ya maisha wananchi wenye kipato cha chini, hasa kwa kuwashushia bei za vyakula na bidhaa mbali mbali.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

48. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ili kutimiza dhamira ya ufugaji wa samaki, Serikali ilikusudia na kuahidi kwamba itazalisha na kusambaza kwa wananchi vifaranga vya samaki milioni 10 kila mwaka kwa watakaojishughulisha na ufugaji wa samaki. Hata hivyo, kasi ya jambo hilo haionekani kwenda sambamba na dhamira ya msingi.

(a) Je, kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023), ni ipi tathmini ya utekelezaji wa dhamira hiyo.

(b) Je, ni ipi takwimu ya mgao wa vifaranga vya samaki kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023) na athari yake katika uzalishaji wa zao la samaki.

(c) Je, ni upi mchanganuo wa aina za vifaranga vya samaki vilivyozalishwa na vilivyosambazwa kwa wananchi kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023).

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

136. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kufuatia Sera na Utendaji wa Rais wa Awamu ya Kwanza Mhe. Abeid Amani Karume katika kuboresha makaazi kwa wananchi wa Unguja na Pemba, kumekuwa na changamoto nyingi katika kuendeleza majengo na nyumba zilizoachwa kupitia sera yake hii.

(a) Je, Serikali inachukuwa hatua gani katika kuhakikisha kunapatikana utekelezaji endelevu wa sera ya makaazi bora na nafuu kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati na matengenezo ya mara kwa mara kwa majengo yaliyojengwa kupitia sera hii, ili kudumisha viwango vya ubora na usalama.

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu katika ujenzi wa nyumba za makaazi bora na nafuu kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba, na ni hatua gani zinazochukuliwa kufanikisha azma hii.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

67. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika ujenzi na matengenezo ya barabara yanayoendelea Unguja na Pemba, kumekuwa na matukio ya ajali na vifo vingi hasa katika barabara ya kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar.

(a) Je, kwa mwaka wa 2023, ni vifo vingapi na ajali ngapi zilizotokea katika barabara inayotoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuelekea Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

(b) Je, ni upi mkakati bora wa kupunguza ajali na vifo vinavyosababishwa na ujenzi na matengenezo ya barabara Unguja na Pemba.

(c) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwalipa fidia wananchi walioumia au kufariki kutokana na ajali zilizosababishwa na ujenzi au utengenezaji wa barabara Zanzibar.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

101. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini iko vipi katika kupungua kwa miti ya mikoko hususani katika maeneo ya Wilaya ya Kati na Kusini Unguja.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Nam. 3 ya 2011 na Kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**15 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**